**EPISODE 10 “WHICH WAY AFRICA?”**

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI:** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu’s restaurant. |
| **MUMBI** | 22 years old, Zapcom’s cousin and social worker. Female. |
| **AUNTIE BONGI** | 45 years old, the local government Telecommunications company manager. Everyone calls him The Manager. |
| **PRESENTER** | Mature woman |
| **SPEAKER** | 45+ ICT Technician |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George’s uncle, owner of KULA TU FOODS. |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

2. **ANNOUNCER** HUJAMBO MPENZI MSIKILIZAJI NA KARIBU KWA MAKALA NYINGINE YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA 'LEARNING BY EAR' NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO,KUHUSU TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO.HII NI MAKALA YA 10 NA YA MWISHO KATIKA MFULULZO WA MCHEZO HUU. KATIKA MCHEZO WA LEO KWA JINA ***"AFRICA KULIKONI?"*** *"WHICH WAY AFRICA?".* ZAPCOM NA WENZAKE WAMEFAULU KUANZISHA BIASHARA YA HUDUMA ZA MTANDAO WA INTANETI KATIKA MKAHAWA WA MJOMBA KILU. KILE KILICHOANZA KAMA CHECHE YA BIASHARA KWA KUTUMIA KOMPUTA MOJA,SASA IMESHIKA KASI NA KUWANUFAISHA WATU WENGI ZAIDI KUTOKANA NA HUDUMA ZA MTANDAO WA INTANETI. LAKINI UPANUZI WA HUDUMA ZA INTANETI KATIKA KIJIJI HIKI, NI MFANO TU WA JINSI HUDUMA HIZI

ZINAVYOENDELEA KUPANUKA BARANI AFICA.

**3. MUSIC:BRIDGE MUSIC**

**SCENE 1: INTERNATIONAL ICT CONFERENCE, NAIROBI KENYA**

**4. A-SFX: NOISE OF SOUND EQUIPMENT BEING TESTED AND PEOPLE GATHERING AT A CONFERENCE. SOUNDS OF RUNNING FEET AND PANTING**

| | | |
|---|---|---|
| **5.** | **GEORGE** | (PANTING) Zap… Zap… uko hapo…! mkutano umeanza ? |
| **6.** | **ZAPCOM** | Habari George, nilijua tu utafika kuchelewa,….! utafika dakika za mwisho mwisho! Tunatafuta mahali pa kuketi. |
| **7.** | **GEORGE** | Shangazi Bongi, habari za asubuhi?.Asante sana kwa kutupatia fursa hii kuhudhuria mkutano huu…! tazama….ooh Mungu wangu…! Watu waliovalia suti za ghali… ehhh ..ehhh .. Mumbi umevalia nadhifu sana!. |

**8.** **MUMBI** Habari George. Umechelewa!. Shangazi Bongi, asante sana kwa kutualika. Ni heshima kubwa sana kwetu!. (**REPRIMANDING)** George… unatuaibisha, si lazima wajue umetoka mashambani..!.Piga moyo konde. Wewe unamiliki mikahawa mikubwa ya huduma za Intaneti.

**9.** **AUNTIE BONGI** Ni kweli!. Labda wewe unajua mengi zaidi kuliko watu wengi hapa na wangependa kujifunza kutoka kwako.Wengi hapa ni mameneja wa teknolojia ya mitandao ya Intaneti kama mimi … lakini wewe … wewe ni mfanyabiashara!! (**CHIDDING**) Na hivi karibuni huenda ukatuajiri watu kama mimi!!

**10.** **ZAPCOM/MUMBI/GEORGE.** **LAUGHTER.**

**11.** **AUNTIE BONGI** Sasa tufanyeni haraka ..tupate mahali tuketi.

12. **B-SFX: MORE SOUND TESTING AND CHAIRS BEING PULLED OUT**

13. **PRESENTER** **(OVER THE PUBLIC ADDRESS SYSTEM)** Mabibi na mabwana, ketini tafadhali!. Programu yetu ni ndefu sana. Msemaji wa kwanza atakuwa mwakilishi wa mradi wa ***TEAMS***. Karibu utujuze mengi kuhusu mradi ya mkonga wa mawasiliano au kwa kitalaam ***Fibre Optic Cable*** ..karibu!

14. **ZAPCOM** **(LOUD WHISPER)** ***TEAMS*?**

15. **AUNTIE BONGI** **(LOUD WHISPER)** Maana yake ni mradi unaokusudiwa kuunganisha eneo la Afrika Mashariki na huduma za Intaneti kwa kutumia nyaya zinazopitia chini ya bahari.Ni mradi unaofadhiliwa na mataifa mbalimbali ili kuunganisha huduma hizo za Intaneti kupitia nyaya nyambizi kutoka Fujaira katika milki za Kiarabu hadi mjini Mombasa.

**16.** **GEORGE** **(LOUDER WHISPER)** Hebu rudia tena ***fibre optic*** ni nini?

**17.** **B-SFX: A SPEECH GOES ON IN THE BACKGROUND**

**18.** **MUMBI** **(LOUD WHISPER)** Unapiga kelele George, na hakika msemaji atazungumzia suala hilo....tumsikilize...!

**19.** **SPEAKER** **...** Bara la Afrika na hasa mataifa yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara yamebaki nyuma sana ikilinganishwa na mabara mengine ulimwenguni katika maendeleo ya huduma hizi za Intaneti zinazopitia chini ya bahari, kuunganisha mabara, nchi na nchi au hata ndani ya nchi moja..

**20.** **ZAPCOM** Shangazi kwa hivyo una maana huduma hizi ni za gharama nafuu katika mataifa mengine?

**21.** **AUNTIE BONGI** Ndio tena sana.

**22. GEORGE** **(LOUD WHISPER)** Lakini bado sielewi maana ya ***fibre optic***.

**23. C: SFX. GEORGE LETS OFF A SCREAM. SOMEONE DEMANDS SILENCE BY SAYNG SHHHHH.**

**24. GEORGE** Mumbi, kwa nini unafanya hivyo? Mbona umenivuta nywele?

**25. MUMBI** Hebu fikiria unene wa unywele wako na uwe na uwezo wa kubeba mamilioni ya nyaya ndogo ndogo!.Nyaya hizi huwezesha mawasiliano kupeperushwa katika masafa marefu kwa kasi sana…. Huo ni mfano mzuri wa ***Fibre optics,***

**26. AUNTIE BONGI** **(REPRIMANDING)** Nyinyi wawili, tafadhali nyamazeni msikilize.

**27.** **SPEAKER** …na wale ambao bado wanajiuliza masuali kwa nini tutumie nyaya nyambizi. Hii ni kwa sababu teknolojia hii ya kutumia nyaya nyambizi badala ya nyaya za kawaida, ni kwa sababu hupeleka mawasiliano mbali zaidi bila ya kupoteza ubora wake. Na pia si rahisi kuathiriwa na sumaku ya umeme!.

**28.** **AUNTIE BONGI (WHISPHERING)** George,kwa hiyo huduma hizi za kutumia mkonga wa mawasiliano yaani ***Fibre Optic*** ni muhimu kwa kuongeza kasi ya kufungua, kupokea na kutuma habari katika komputa.

**29. SPEAKER** **(OVER THE PUBLIC ADDRESS SYSTEM)...**Ukosefu wa mfumo huu wa mtandao wa Intaneti ambao ni bora zaidi, ndio chanzo cha kupanda kwa gharama na huduma za polepole katika mataifa mengi barani Afrika. Na zaidi, si mataifa mengi yaliyounganishwa na mfumo huu wa mtandao, ambao ungeboresha huduma hizi na kuyawezesha mataifa mengi barani Afrika kuwasiliana kwa urahisi na mataifa ya bara Ulaya na Marekani kuliko ilivyo sasa baina ya mataifa jirani barani humu!.

**30. ZAPCOM** **(WHISPERING)** Maskini Afrika... na hiyo ndiyo hali halisi miongoni mwa mataifa mengi ya Afrika?

**31. AUNTI BONGI** Shhhh…Labda msemaji atalizungumzia suala hilo pia…. msikilize!

**32. ANNOUNCER** Ndilo suala lililosisitizwa na msemaji mmoja baada ya mwengine katika mkutano huo.Washiriki walibadilishana mawazo kuhusu teknolojia mpya ya habari na mawasiliano na njia za kuboresha huduma hizi za mtandao wa Intaneti barani Afrika. Mengi yamezungumzwa kuhusu sekta hii ya habari na mawasiliano katika kipindi cha muda mfupi.Bila shaka ZAPCOM, MUMBI na GEORGE wana maswali mengi ya kumuuliza shangazi Bongi. Na bila ya kupoteza wakati wote wanaandamana moja kwa moja hadi mkahawa mmoja ili kulijadilia suala hili kwa kina zaidi.

**33. MUSIC:BRIDGE MUSIC**

**SCENE TWO-COFFEE HOUSE**

**34. GEORGE** Ohh mungu wangu!, huu mkahawa unapendeza na kuvutia sana. Si kama ule wetu wa Kula Tu Foods!

| | | |
|---|---|---|
| **35.** | **ZAPCOM** | George, hapa ni jijini .Shangazi Bongi hebu tueleze sababu ya kuanzisha miradi hii yote. Kwa kweli suala hili linanitatanisha sana! |
| **36.** | **AUNTIE BONGI** | Mradi wa kuunganisha bara la Afrika na huduma hizi za mtandao wa Intaneti kwa kutumia nyaya nyambizi ni wa gharama sana.Ni lazima nyaya hizi zipitishwe chini ya bahari. Kwa hivyo kadri watu wengi wanavyowekeza katika mradi huu, ndio manufaa yake yanavyozidi bara Afrika. |
| **37.** | **MUMBI** | Kwa nini basi hawajaukamilisha? |
| **38.** | **AUNTI BONGI** | Ohhh, lakini hawajashindwa...! wanakaribia na hata kwa kiwango fulani tayari wengine wamafaulu. Pia lazima ufahamu kwamba kuna mikataba baina ya mataifa ya Afrika na mabara mengine na mikataba hii mara nyingi huchukua muda mrefu kutekelezwa. |

**39. ZAPCOM** Ni jambo zuri kuwa na teknolojia hii ya mkonga wa mawasiliano , lakini itakuwa na maana gani kama watu bado hawana uwezo wa kumudu Komputa au simu za mkononi?.

**40. AUNTIE BONGI** Swali zuri sana. Naamini, ingawa mimi si mtaalam wa masuala hayo, hii ndiyo sababu mataifa mengi barani Afrika sasa yameanza kuondolea mbali ushuru unaotozwa Komputa na bidhaa zake zinazoagizwa kutoka nje.

**41. GEORGE** Hilo ni jambo zuri sana.

**42. MUMBI** Endapo serikali haitabadilisha msimamo wake kuhusu suala la ushuru unaotozwa bidhaa hizi, basi pia sisi tutaweza kuagiza na kuuza Komputa na kupata faida nzuri.

**43. ZAPCOM** Hebu tuendelee kunywa!

**44. MUMBI** Ndio tusherehekee ….heko Afrika!.

**45. AUNTIE BONGI** Ndio….. tunywe kusherehekea teknolojia mpya ya mawasiliano na maendeleo ya huduma za Intaneti barani Afrika.

**46. GEORGE** Pia tunywe… kusherehekea ufanisi wa biashara yetu. Lakini tunapaswa kwenda nyumbani sasa!. Na hakika mjomba Kilu sasa amaenza kuwa na wasiwasi.

**47. ANNOUNCER** Kundi hili la vijana bado lina mengi ya kutafakari. Sasa wanaelekea nyumbani wakiwa na lengo moja tu la kutafuta njia ya kuboresha biashara yao na huduma za teknolojia mpya ya mawasiliano.Wamekuwa na wakati mzuri kujifunza mengi katika mkutano huo.

**48. MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE THREE. KULA TU FOODS; SFX: FOOT STEPS**

**49. GEORGE** Mjomba Kilu, tumerejea!. Ni furaha yetu kurudi tena katika mkahawa huu wa Kula Tu Foods.

**50. UNCLE KILU** Mumetamani chakula ch hapa. Basi leo nimemutengenezea supu tamu sana ya mbuzi. Zapu... mbona umenyamaza.

**51. ZAPCOM** Mjomba, kuna mambo mengi sana yanayonisumbua akili!.

***52.*** **UNCLE KILU** Kwanza kunywa supu, kisha uniambie kinachokusumbua. Unajua mara nyingi mtu hawezi kufikiria viruzi au kufanya chochote kama matumbo yake yananguruma. Wakati unaposhiba basi hapo tunaweza kuzungumza! **(PAUSE)** George, tafadhali nenda ukaitengeneze ile komputa nambari 5 inatusumbua sana. ***Reboot***

**53. ZAPCOM/MUMBI/GEORGE** Nini?

**54. GEORGE** Weee... weee... mjomba umesema ***reboot?***

| | | |
|---|---|---|
| **55.** | **UNCLE KILU** | **(DISMISSIVELY)** Kwani unafikiri nimekuwa nikifanya nini wakati wote mlipokuwa mumeondoka kwenda jijini.. (**PROUDLY)** Nilikuwa nikisimamia biashara hii. |
| **56.** | **MUMBI** | Mjomba huishi kutushangaza. |
| **57.** | **UNCLE KILU** | Sasa, Zapu…! niambie kinachokusumbua huku unapoendelea kunywa supu. |
| **58.** | **ZAPCOM** | Ni jambo la kutatanisha sana ….kuna mambo mengi tu yanayoendelea barani Afrika kuhusu masuala ya Komputa, Intaneti na sekta nzima ya mawasiliano. |
| **59.** | **UNCLE KILU** | Kweli? |
| **60.** | **ZAPCOM** | Sijui nianzie wapi |
| **61.** | **UNCLE KILU** | Msingi ni upate chanzo chake. |
| **62.** | **ZAPCOM** | Sijui … chanzo chake ni nini? |
| **63.** | **UNCLE KILU** | Unaweza kuanzia katikati, mbele na au nyuma kadri utakavyo wewe mwenyewe. Unafikiria nini? |

| | | |
|---|---|---|
| **64.** | **ZAPCOM** | Mzee… Tumepata maendeleo makubwa sana katika kijiji chetu. Lakini kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotumia Komputa zetu na kununua kadi za simu, haitoshi, kuna mengi ya kujifunza katika matumizi ya Komputa na simu za mkononi ili kurahisisha maisha yao na kuboresha zaidi huduma hizi. |
| **65.** | **UNCLE KILU** | Lakini hadi kufikia sasa mimi sijaona tatizo lolote! |
| **66.** | **ZAPCOM** | Lakini wanahitaji kupata mafunzo zaidi jinsi ya kutumia vyema huduma hizi. |
| **67.** | **UNCLE KILU** | Wafunze basi. |
| **68.** | **ZAPCOM** | Lakini nina kazi nyingi sana |
| **69.** | **UNCLE KILU** | Fanya ualimu iwe biashara yako. Aaahhh… Vijana wa siku hizi!. Haya basi maliza supu yako haraka na uwaite wenzio muanzishe chuo hicho mara moja. Na kumbuka nitakuwa mlikaji mkubwa wa hisa katika chuo hicho. |

**70.** **ZAPCOM** Sawa mjomba, shule ya … (THOUGHFUL) ***Kilu School of Technology***….nalipenda jina hilo.

**71.** **UNCLE KILU** Kunywa supu yako!. Ni nzuri, hufanya mtu kuwa mwerevu sana.

**72.** **MUSIC:THEME MUSIC**

**OUTRO**

**73.** **ANNOUNCER** Imebainika kuwa teknolojia hii ni fursa nzuri ya kuleta maendeleo katika kijiji hiki. Lakini yote itategemea kujitolea kwa watu binafsi. Bila shaka vijana ambao watatumia vyema fursa hii watakuwa na mengi ya kujifunza. Lakini kwa wale ambao hawatajishughulisha na chochote ila kunung'unika kwamba bara la Afrika liko nyuma kimaendeleo huku wakiendelea kulilinganisha na mataifa yaliyostawi, hapana shaka wataendelea kubakia nyuma miaka nenda miaka rudi!.Maendeleo ni

suala la kila siku na yanahitaji juhudi za kila mmoja wetu.Hivyo watu wanapasa kujikakamua kutumia kila fursa iliyopo kujiendeleza.. ZAPCOM na kundi lake wamefahamu hilo, na kama washirika wa kibiashara wamebadili maisha miongoni mwa wakaazi wa kijiji chao..

Je na wewe unafanya juhudi gani kuona kwamba unaenda na wakati katika Teknolojia hii mpya ya mawasiliano na Mtandao wa Intaneti?

Hiki kilikuwa kipindi cha 10 na cha mwisho katika mfululizo wa vipindi hivi vya mchezo wa redio kuhusu teknolojia mpya ya habari na mawasiliano na Mtandao wa Intaneti.Ukipenda kusikiliza tena tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa Sasa.